



## Utangulizi

Upatanisho ni tendo ambalo Mungu na mwanadamu wanaletwa pamoja katika mahusiano ya kipekee. Neno la Kiingereza linalotumika linatokana na lugha ya Ki Anglo Saxon, ambayo ni lugha ya kale iliyotumika Uingereza yenye maana 'kufanyika kuwa kitu kimoja'. Hivyo kuna baadhi ya watu wamesema upatanisho maana yake ni 'kufanyika kuwa kitu kimoja'. Maana hii ya upatanisho inaashiria kuwepo kwa hali ya utengano – na hali hii ya utengano inapaswa kushindwa ikiwa tutamfahamu Mungu na iwapo tutakuwa na faragha naye. Neno 'upatanisho' katika Agano la Kale ni 'Kaphar' (kufunika), hii ina maanisha ya kwamba dhambi zimefunikwa kwa njia ya damu ya sadaka. Katika theologia, neno 'upatanisho' limefikia mahali na kuongeza maana ikiwa ni pamoja na kumaanisha taswira ya ukombozi kupitia damu ya Kristo. Neno hili linatumika mara moja katika Agano Jipya katika Warumi 5:11, ila katika tafsiri mpya limetafsiriwa kama 'upatanisho' ambalo ni neno linaloleta maana zaidi katika lugha ya kisasa.

Haja ya kuwa na upatanisho inatokana na hali ya mwanadamu kulevywa na dhambi. Biblia yote inatuonyesha juu ya dhambi zetu. Baadhi ya mifano ni kama ifuatavyo:

Isaya **53:6** - Sisi sote kama Kondoo tumepotea

Yeremia - **17:9** Moyo wa mtu ni mdanganyifu kuliko vitu vyote; hauwezi kuponywa, hakuna awezaye kuelewa

Zaburi **14:3** - Lakini wote wamekosa, wote wamepotoka pamoja; hakuna atendaye mema, hakuna hata mmoja.

Warumi **3:23** – Kwa maana wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu

Mtume Paulo alieleza juu ya maadui wa Mungu (Warumi **5:10**), wamejiwekea uadui na Mungu, (Warumi **8:7**), wamejitenga na kuweka uadui akilini mwao (Wakolosai **1:21**)

## Katika kipindi cha Agano la Kale

– Dhambi zilifunikwa na Mungu huku akitazamia ujio wa msalaba. Sadaka ilikuwa ndio dawa ya dhambi, na mtu alitoa sadaka si tu kwa dhambi zake ila kwa dhambi za familia yake. Anapokuwa ametubu kweli, alitoa sadaka ya mnyama asiye na hatia – na kila mara mnyama huyo alipaswa kutokuwa na dosari yoyote. Aliamini kuwa Mungu angetimiza ahadi yake kwa kumsafisha dhambi zake zote, kama angemwaga damu.

Kutoka **30:10**; Waebrania **10:4**; Mambo ya Walawi **1:3-4**; **4:27-31**; **16:11, 17, 30**; **17:11**; **23:27**

## Sadaka za wanyama zilikuwa ni maandalizi ya sadaka ya Yesu

Kwa namna fulani zinaweza kudhaniwa kuwa ni kielelezo cha kifo cha Yesu Kristo.

Waebrania **10:1**; Yohana **1:29**; 1Yohana **2:2**; Waebrania **9:13-15, 22, 26**; **10:10, 14**;  
Warumi **3:25**; **8:3**; 1 Wakorintho **5:7**

Kwa njia ya neema, tunapokuwa tumetubu dhambi, na tunapoiamini damu ya Yesu iliyomwagika kwaajili yetu, tunakuwa tumepatanishwa na Mungu. Upatanisho unakuwa umefanyika. Upatanisho kwa njia ya damu ya Yesu. Damu yake ilikuwa ni gharama iliyostahili kulipwa kwaajili ya ukombozi wa ulimwengu.

Hivyo tunaposema kifo cha Kristo ulikuwa ndio wakati maalum, na tukio maalum katika historia ya ulimwengu si ushabiki tu ila ni uhakika.

Marko **10:45**; Yohana **10:11**; Warumi **3:21–25**; **5:10, 11**; 2 Wakorintho **5:21**; Waefeso **1:7**;  
1 Petro **1:18-19**; 1 Yohana **4:10**

## Maelezo

Maneno ambayo yanaweza kutumiwa kuelezea juu ya upatanisho:

**Uwakilishi** - Kifo cha Kristo kiliwakilisha (tazama Waebrania **2:14-17** na Warumi **5:19**).

**Kipatanisho** – Kifo cha Kristo kinatufanya tuwe watu ambao vinginevyo isingewezekana kuwa – kinatufanya tukubalike mbele za Mungu (tazama 1 Yohana **4:10**).

**Mbadala** – Kifo cha Kristo kilikuwa ni mbadala – yaani kwakuwa Yesu alifufuka baadala yetu – alichukua nafasi ya mwenye dhambi (tazama Isaya **53:5-6**, na 1 Petro **2:24**).

Copyright © Sovereign World Trust, PO Box 777, TONBRIDGE, Kent, TN11 0ZS, UK  
[www.sovereignworldtrust.org.uk](http://www.sovereignworldtrust.org.uk)

### Publishing and Translation History

First Published in English by Glory to Glory Publications.

Christian Publications International, PO Box 212, Saffron Walden, CB10 2UU - [www.christian-publications-int.com](http://www.christian-publications-int.com)  
Editor Peter Sammons. Contributors Alex Jacob, David M. Moore, Peter Byron- Davies, Greg Stevenson, Peter Sammons  
ISBN English 978-0-9567831-6-5

This Kiswahili translation for Sovereign World Trust by Revd John Y Madinda with permission  
Swahili Edition Published by Sovereign World Trust ISBN - Kiswahili 978-1-908010-12-4